BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tano – Tarehe 18 Septemba, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

141. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tathmini iko vipi juu ya uwiano wa maangamizi ya madawa ya kulevya na ongezeko la matumizi ya madawa hayo siku hadi siku.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

137. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tathmini iko vipi katika kuona kwamba mianya ya rushwa katika miradi ya maendeleo ya kimkakati inadhibitiwa.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

233. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ina mkakati gani wa kuondoa changamoto ya uchache wa vitendea kazi vya kuondoa uchafu mitaani.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

45. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

(a) Tathmini iko vipi kwa sasa juu ya idadi ya wafanyakazi wa majumbani katika Falme za Nchi za Kiarabu wanaotokea Zanzibar.

(b) Ni kwa kiasi gani na utaratibu upi Serikali imekuwa ikiufanya katika kusikiliza changamoto za wafanyakazi hao na kuzipatia ufumbuzi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

256. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kuna fursa nyingi wanazozipata watumishi ambao wamepata ithibati katika fani ya uhasibu kama vile CPA na ACCA tofauti na wale wenzao ambao wamepata ithibati kwenye fani ya ununuzi mfano wa CPSP, CSP na CIPS. Jambo hili limewafanya wataalamu wengi wa kada ya ununuzi kukata tamaa ya kutojiendeleza kutafuta ithibati hizi ambazo ni muhimu kwa kada hii kwa maendeleo ya nchi yetu.

(a) Je, kwa takwimu ni wataalamu wangapi wa Kada ya Ununuzi wana ithibati na ni chombo gani kilicho na wajibu wa kusajili wataalam wa Kada ya Ununuzi hapa Zanzibar.

(b) Je, ni yepi maslahi wanayopata watumishi walio na ithibati katika Kada ya Ununuzi.

(c) Je, Serikali inachukua juhudi gani ili kuwashajihisha watumishi kutafuta ithibati hizi ambazo ni muhimu katika kuongeza ufanisi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

73. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kiasi gani lengo halisi la kudumisha na kuendeleza tamasha la utamaduni wa kizanzibari linafikiwa.

75. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Je, kwa nini iliyokuwa TVZ ni miongoni mwa Televisheni zenye historia ya kipekee katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa jangwa la Sahara.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

7. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitisha Sheria ya Adhabu ya papo kwa papo kwa wananchi wote ambao wanafanya makosa barabarani.

(a) Ni makosa ya aina gani wananchi wanapaswa kutozwa adhabu ya papo kwa papo.

(b) Ni taratibu zipi mtoa adhabu anapaswa kuzifuata wakati wa kutoa adhabu hizo.

(c) Ni nani hasa anapaswa kutoa adhabu hizo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

232. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi na bidii kubwa katika kuboresha Sekta ya Elimu Zanzibar. Hata hivyo kuna baadhi ya skuli za zamani zipo kwenye hali mbaya na kuna uhaba mkubwa wa vitendea kazi, tatizo ambalo pia linaiathiri Skuli ya Msingi ya Kiembesamaki.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati skuli hizo.

(b) Ni lini Skuli ya Msingi ya Kiembesamaki B itatengenezwa na kupatiwa vitendea kazi vya kutosha.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

226. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Sekta ya Kilimo hususani kilimo cha juu (maweni) kinakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa huduma ya ushauri wa mabibi na mabwana shamba kwa wakulima. Hali hii husababishwa na kukosekana kwa usafiri (vipando) kama vile pikipiki na baskeli kwa ajili ya kuyafikia maeneo hayo.

Je, ni lini Serikali itawapatia mabibi na mabwana shamba vipando vya kutosha, ili wakulima wa maweni waweze kuimarisha kilimo hicho.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

74. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Miji mipya mbali mbali imekuwa ikiibuka nje kidogo na kandokando ya jiji la Zanzibar.

Je, Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) lina utaratibu upi wa kuweka transfoma zenye uwezo na ubora wa kukidhi haja ya ongezeko la makaazi mapya ya watu katika miji hiyo.

**Wizara ya Afya:**

222. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya watu katika Kijiji cha Maafa kilichopo katika jimbo la Nungwi, kumepelekea huduma za afya katika kijiji hicho kuzidiwa na kutokidhi haja kwa wanajamii husika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukijenga Kituo cha Afya cha kijiji hicho, ili kuwaondoshea usumbufu wanajamii wa eneo hilo na Nungwi kwa ujumla.

273. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa tiba asili ni tiba inayotambulika katika nchi zinazoendelea, ambapo Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kuwa zaidi ya asilimia 30% ya watu kutoka katika mataifa yanayoendelea wanatumia tiba asilia na tiba mbadala katika kukabiliana na maradhi ya aina mbali mbali.

(a) Je, ni wataalamu wangapi wa tiba asili na tiba mbadala wamesajiliwa Zanzbar.

(b) Je, Serikali inatumia utaratibu upi wa kusajili watalamu wa tiba asili na tiba mbadala Zanzibar.

(c) Je, ni utaratibu upi unaotumika katika kutoa matangazo ya tiba asili na tiba mbadala katika mitandao ya kijamii na mabango mitaani.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**18 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**